JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**31 Machi 2026**

# TAARIFA KWA UMMA

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA WAELIMISHAJI WALIOTHIBITISHWA WA ELIMU YA FEDHA

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kama Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Kifedha, kwa kushirikiana na wasimamizi wengine wa sekta ya fedha, ilizindua Mtaala wa Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha (Certified Financial Educators-CFE) mwezi Desemba 2023. Programu ya Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha ilianzishwa ili kukabiliana na changamoto ya uelewa mdogo wa masuala ya kifedha kwa watu walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Programu hii inatekelezwa kupitia Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Benki Kuu ya Tanzania na taasisi za elimu, mafunzo na utaalamu ilizoziainisha, kwa lengo la kuweka ulinganifu katika utoaji wa elimu ya fedha, kuboresha ufanisi, na kuimarisha uratibu wa utoaji wa elimu ya fedha nchini kwa kutumia majukwaa ya kitaaluma na mafunzo.

Tangu kuanza kwa utekelezaji wake, zaidi ya watu 1,388 wamethibishwa na kwa sasa wanatoa elimu ya fedha kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali kama vile semina, mikutano na mitandao ya kijamii. Matokeo ya awali yanaonesha mabadiliko chanya katika tabia za kifedha, hususani katika kuzifikia na kuzitumia bidhaa na huduma za akiba pamoja na uwekezaji.



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501

Licha ya mafanikio haya, kumekuwa na changamoto kuhusu mwenendo wa baadhi ya Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha ambao wamekuwa wakitoa taarifa zisizo sahihi au kuwasilisha vibaya malengo ya programu. Hivyo, Benki Kuu inawakumbusha Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha kuzingatia masharti yafuatayo:

(i) Kuzingatia maadili na malengo ya programu;

(ii) Kufundisha kanuni na maudhui waliyofundishwa na kuthibitishwa;

(iii) Kutumia majina na utambulisho rasmi wa programu ili kuepuka kuwasilisha vibaya utambulisho wao kwa umma;

(iv) Cheti cha Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha sio hadhi ya kuwa taasisi ya fedha, mfanyakazi wa Benki Kuu ya Tanzania, dalali wa Masoko ya Fedha, Kocha, au Mshauri wa masuala ya fedha; na

(v) Kueleza sifa zingine za kitaaluma walizonazo kutoka taasisi zinazotambuliwa.

Benki Kuu, kwa kushirikiana na taasisi za elimu, mafunzo na utaalamu ilizoziainisha, haitasita kuchukua hatua stahiki ikiwemo kufuta cheti cha mhusika endapo kutakuwa na ukiukwaji wa masharti haya.

Aidha, Benki inaendelea kuthamini na kutambua mchango mkubwa wa Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha katika utoaji wa elimu ya fedha kwa umma, na inatoa wito wa kuendelea kudumisha taaluma, uadilifu na kuzingatia kikamilifu malengo ya programu.

**Emmanuel M. Tutuba**

**GAVANA**

BENKI KUU YA TANZANIA
1966-2026



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501